**OFISI YA RAISI (TAMISEMI)**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA**

SHULE YA SEKONDARI NAMWAI,
S. L P 174,
SANYA JUU, SIHA.
28/03/2022

MZAZI/ MLEZI WA ………………………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA NAMWAI**

Jumuiya ya shule ya sekondari Namwai inayofuraha kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha tano kwa mwaka wa masomo **2022/2023**, hongera sana. Mwanafunzi atatakiwa kuripoti tarehe itakayopangwa kuanzia saa nne asubuhi hadi saa kumi na moja kamili jioni na mahitaji yote yaliyoainishwa.

## 1. MAHALI SHULE ILIPO

Shule ya Sekondari Namwai ipo katika Kata ya **Ngarenairobi** wilaya ya Siha Mkoa wa Kilimanjaro kilomita 16 kutokea mji mdogo wa **Sanya Juu**. Ukitokea **Moshi** mjini unapanda magari yanayo elekea **Sanya Juu** kwa gharama ya shilingi **2,000/=** (Kwa wanaotokea Arusha Mjini wanashuka kituo cha mabasi **Boma Ng'ombe** na kisha kupanda mabasi yanayoelekea Sanya Juu kwa gharama ya shilingi 1,000/=). Kutoka Sanya Juu stendi unapanda magari yanayoelekea **Ngare - Matadi** na kushuka kituo cha **Shule ya Sekondari Namwai** kwa gharama isiyopungua shilingi 1000/= kwa usafiri wa Noah au daladala.

## 2. ADA, MICHANGO NA MICHANGO YA SHULE

| NA | MAHITAJI | KIASI CHA MALIPO | MAELEZO | AKAUNTI NAMBA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ada | 70,000/= | Kwa mwaka | 4011200102 NMB |
| 2 | Matroni na Patroni | 20,000/= | Kwa mwaka | 40102300901 NMB |
| 3 | Mpishi | 20,000/= | Kwa Mwaka | 40102300901 NMB |
| 4 | Mlinzi | 20,000/= | Kwa Mwaka | 40102300901 NMB |
| 5 | Taaluma | 20,000/= | Kwa Mwaka | 40102300901 NMB |
| 6 | Huduma ya kwanza | 10,000/= | Kwa Mwaka | 40102300901 NMB |
| 7 | Ukarabati | 15,000/= | Kwa Mwaka | 40102300901 NMB |
| 8 | Kitambulisho | 5000/= | Kwa Mwaka | 40102300901 NMB |
| 9 | Nembo | 3000/= | Kwa Mwaka | 40102300901 NMB |
| 9 | Tahadhari | 5,000/= | Kwa Mwaka | 40102300901 NMB |
| | Jumla | **188,000/=** | | |

**N.B.**

Malipo yote yafanyike katika account za benki zilizoanishwa na Mwanafunzi anapokuja shuleni aje na ***pay- in slip*** kwa uthibitisho. Hakuna fedha itakayopokelewa shuleni. Jitahidi kufanya malipo yako kwa wakati.

**2.1 SARE (UNIFORM)**

**KWA WASICHANA**

1. Sketi mbili za rangi ya kijivu-iliyokolea (grey) rinda boksi urefu wa sentimita 16 kutoka kwenye goti kwenda chini, Mashati mawili meupe ya mikono mirefu na soksi- nyeupe ndefu jozi mbili au zaidi .**Sketi fupi haziruhusiwi**.
2. Sweta mbili za rangi ya kijivu-iliyokolea (grey).
3. Gauni mbili za kushindia za kitambaa kizito cha draft ndogo za rangi ya maroon mshono wa solo. Ziwe ndefu sentimita kuanzia 16 chini ya goti.
4. Sketi moja nyeusi ya mshono wa solo na ***skintight mbili*** ndefu nyeusi za michezo
5. T. shirt mbili za bluu iliyokolea yenye kola kwa darasani.
6. Sweta mbili nyeusi nzito zisizo na maandishi au alama nyingine yoyote kwa ajili ya baridi.
7. Soksi ndefu nyeusi nzito na pulneck (sweta kabashingo) rangi nyeusi kwa ajili ya baridi.
8. Viatu vyeusi vya Kamba pea mbili vyenye kisigino kifupi, raba-nyeusi za michezo na Mabuti kwa ajili ya matope wakati wa mvua.
9. Track-suit nzito rangi ya kijivu isiyobana.

**KWA WAVULANA**

1. Suruali mbili za rangi ya kijivu iliyokolea (grey) yenye rinda, Mashati mawili meupe ya mikono mirefu na soksi nyeusi
2. Sweta mbili za rangi ya kijivu-iliyokolea (grey)
3. Suruali mbili nyeusi na tshirt 2 za rangi ya kijivu iliyokolea (grey) (aina ya form six) Isiwe na maandishi, alama au rangi yoyote ya ziada.
4. Sweta mbili za rangi ya kijivu-iliyokolea (grey).
5. Jezi moja ya michezo (tshirt na bukta) za rangi nyeusi yenye *strips* nyeupe
6. T. shirt mbili za bluu iliyokolea yenye kola (aina form six) kwa darasani
7. Sweta mbili nyeusi nzito zisizo na maandishi au alama nyingine yoyote kwa ajili ya baridi.
8. Soksi ndefu nyeusi nzito na pulneck (sweta kabashingo) rangi nyeusi kwa ajili ya baridi.
9. Viatu vyeusi vya Kamba pea mbili vyenye kisigino kifupi, raba-nyeusi za michezo na Mabuti kwa ajili ya matope wakati wa mvua.
10. Track-suit nzito rangi ya kijivu isiyobana.

## 2.2 MAHITAJI MENGINE

Mwanafunzi anapokuja shuleni aje na vifaa vifuatavyo:-

- Sanduku imara la chuma na kufuli
- Blanketi moja zito
- Mashuka mawili ya rangi ya ***Light blue*** na foronya mbili za rangi hiyo hiyo Wavulana na Wasichana.
- Bedcover/Shuka moja nyeupe na foronya yake nyeupe kwa wavulana na wasichana
- Ndoo ndogo moja na kubwa moja
- Tochi ya betri au sola
- Scientific calculator ***fx992*** na kuendelea na **dissecting-kit moja**
- Madaftari saba ***counter books Quire 3/4*** na daftari ndogo (Msomi) saba za mazoezi
- Sahani, kijiko na vikombe vya bati au mfupa. Vyombo vya plastic havitaruhusiwa kabisa.
- Mwanafunzi aje na *fyekeo, hard broom, soft broom, squeezer, jembe na mpini* .
- Sabuni ya maji lita 5 kwa ajili ya usafi vyooni
- Rimu 1 (A4) kwa mhula
- Paspoti size moja ya rangi.
- Vitabu vya tahasusi atakayosoma mwanafunzi.
- Kukodisha godoro kwa mwaka mmoja Tsh. 15000/= au mwanafunzi anaweza kuja na godoro lake.

## 4. MATIBABU

Wanafunzi wenye bima waje na bima zao. Wanafunzi wasio na bima ya afya mzazi/mlezi ajitahidi kumkatia bima kubwa (NHIF). Edapo mzazi/mlezi atashindwa kumkatia bima hiyo, aje na kiasi cha Tsh 50,400/= uongozi wa shule utashughulikia upatikanaji wa bima hiyo itakayotumika kwa mwaka moja tu.

Taarifa ya tatizo lolote la kiafya la mwanafunzi liwe na uthibitisho wa daktari. Mwanafunzi ampatie matron/patron uthibitisho huo mara anaporipoti shuleni. Endapo mwanafunzi amelazwa hospitali atarudi mara tu atakaporuhusiwa na daktari na kuripoti kwa matron/patron. Matibabu makubwa yasiyotumia bima yatagaramikiwa na mzazi au mlezi.

## 5. VIFAA VYA USAFI BINAFSI

Mwanafunzi aje na sabuni, taulo, kandambili, rangi ya viatu vyeusi, brash ya viatu, mswaki, dawa ya meno, mafuta ya kupaka ya mgando (aina ya Vaseline au Babycare) na nguo za ndani za kutosha. Mafuta ya kupaka aina nyingine, cream na marashi haviruhusiwi kabisa shuleni.

## 6. ORODHA YA VITABU

Kutokana na uhaba wa vitabu, mzazi/mlezi anashauriwa kumnunulia mwanae vitabu vitakavyomsaidia katika rejea na mazoezi mengine kulingana na mchepuo anaosoma kwani

vitabu vilivyopo havitoshelezi kila mwanafunzi kupata kitabu chake mwenyewe. Baadhi ya vitabu hivyo ni kama vifuatavyo:-

ADVANCED MATHEMATICS.

1. Advanced Level Pure Mathematics, Fourth Edition by C. J.Tranter
2. Pure Mathematics, by J.K Backhouse
3. Engineering Mathematics sixth edition by K. A.STROUD
4. Advanced Mathematics1-review (problems & solutions)

BASIC APPLIED MATHEMATICS:

1. Additional and Applied Mathematics by J. F.TALBERT
2. Basic applied mathematics (BAM) by Respicius Kiiza and Lugano Mwanginde
3. Basic applied mathematics review questions and solutions

BIOLOGY

1. Biology by S.Chand
2. Biological science by D.J.Taylor
3. Biology for form V&VI by TIE
4. Biology Questions and answer
5. Biology for Advanced level, new understanding,4th Edition by Gleen & Susan Toole

CHEMISTRY

1. Conceptual Chemistry1 &2 (S. Chand)
2. Chemistry in action (Michael Fremantro)
3. Advanced chemistry by Michael Clugston, Rosalind Flemming
4. Comprehensive approach to advanced level CHEMISTRY questions with answers by Sedrick C. Magas, & Kira Ernest
5. Physical chemistry with General chemistry (Advenced) by Mark Daniel Hermes Daniels.

PHYSICS

1. Advanced level physics7th Edition by Nelkon and Parker
2. Advanced physics by Sterv Adams and JonathanAllday
3. Advanced physics review
4. Principle of physics by Chand

GENERALSTUDIES

1. Understanding General Studies For Advanced Level by Bigiwamungu & Deogratius
2. Contemporary Approach for advanced level general studies notes (form 5 & 6) Nyambari Nyagwine

**7. MWENENDO NA TABIA**

- Kila mwanafunzi anawajibu wa kuonyesha kiwango cha juu cha nidhamu katika kila shughuli kama vile kuwahi, ukakamavu, usafi, uaminifu, michezo na kila jambo linalomhusu.
- Mwanafunzi anapaswa kuwaheshimu na kuwatii walimu, wafanyakazi wasio walimu, Wageni na walezi wengine shuleni na nje ya shule.
- Mwanafunzi anapaswa kuwaheshimu viranja wa shule walioteuliwa na kuchaguliwa na wanafunzi wanzake ndani na nje ya shule.

**8. NJE NA NDANI YA MIPAKA SHULE**

- Hairuhusiwi kwenda nyumba za walimu na watumishi wasio walimu bila ruhusa au sababu za msingi.
- Hairuhusiwi mwanafunzi wa kike kufika kwenye mabweni ya wavulana wala mwanafunzi wa kiume kufika kwenye mabweni ya wasichana
- Hairuhusiwi kuingia baa, vilabu vya pombe na nyumba za kulala wageni
- Hairuhusiwi mwanafunzi kulala au kutoka nje ya shule bila kibali cha mkuu wa shule wakati wowote

**9. MAMBO YALIYOPIGWA MARUFUKU SHULENI**

- Kuonesha tabia mbaya kama vile kupigana, kupiga kelele ovyo, kutukana, ulevi wa aina yeyote na tabaia nyingine zingine zisizofaa
- Kukashifu dini yeyote au kabila la mtu
- Kubadili dini
- Kushabikia chama chochote cha siasa
- Kuhamasisha migomo au vurugu ya aina yeyote
- Kukaribisha wageni pasipo idhini ya shule
- Kumkaribisha mgeni au mwanafunzi yeyote asiyehusika bwenini
- Kuharibu mali ya shule, umma au ya mwenzako kwa makusudi
- Kuweka dawa au kusuka nywele, kufuga kucha au kuweka rangi
- Kuvaa/kuja na nguo zisizoidhinishwa kwa matumizi hapa shuleni
- Kuvaa nguo ya mwanafunzi mwingine
- Kumiliki simu ya mkononi, line ya simu au simu yeyote bila idhini ya mkuu wa shule au matron/patron
- Kutumia simu yoyote kuwasiliana na mzazi/mlezi isipokuwa simu ya mkuu wa shule na matron/patron.
- Kuja na vifaa vyovyote vinavyotumia umeme
- Kuchelewa kuripoti shuleni baada ya likizo. Muda wa kuripoti shuleni baada ya likizo ni kabla ya saa 11:00 jioni. Baada ya hapo mwanafunzi hatapokelewa.

## 10. BAADHI YA MAKOSA YANAYOMFUKUZISHA MWANAFUNZI SHULENI

1) Wizi
2) Kuwa na mahusiano ya kimapenzi
3) Uasherati
4) Kupata mimba
5) Kutumia kilevi cha aina yeyote
6) Kumiliki vifaa vyovyote vinavyotumia umeme
7) Makosa ya jinai
8) Kupiga au kupigana
9) Kuharibu makusudi mali ya umma
10) Kudharau bendera ya Taifa, picha ya Rais au Mwenge wa Uhuru
11) Kuoa/Kuolewa
12) Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo
13) Kumiliki simu au line ya simu shuleni
14) Lugha ya matusi
15) Kugoma na kukataa adhabu
16) Kutoroka au kuondoka shuleni bila ruhusa ya mkuu wa shule.
17) Na makosa mengine ya jinai kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi

## 11. MAWASILIANO

Mawasiliano yote yafanyike kwa namba za simu zifuatazo:
Namba ya simu ya mkuu wa shule: 0688154873
Namba ya simu ya makamu mkuu wa shule: 0757504422/0754641005
Mwanafunzi anapaswa kujaza fomu ya matibabu na taarifa binafsi.
Ninakutakia safari njema ya kufika hapa shule ya sekondari Namwai. Karibu sana.

Anna J. Urassa
Mkuu wa shule

**THE PRESDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**SIHA DISTRICT COUNCIL**
**NAMWAI HIGH SCHOOL**

MEDICAL EXAMINATION

(To be completed by a medical Officer in respect of all form I and 5 entrants)

Pupil's full name ……………………………………………………………………………………………………………………………….

Age ………………………………………………………………………………………………………………………………………………….

Blood count (red and white) ……………………………………………………………………………………………………..……

Stool examinations …………………………………………………………………………………………………………..……….

Urinalysis ………………………………………………………………………………………………………………..……,,,,………….

Syphilis test ……………………………………………………………………………………………………..…………………….

T.B.test ………………………………………………………………………………………………………………………………………

Eye test ……………………………………………………………………………………………………..…………………….

Ears ……………………………………………………………………………………………………………………………………………..

Chest ……………………………………………………………………………………………………………………………………...

Abdomen …………………………………………………………………………………………………………………………………..

Spleen ………………………………………………………………………………………………………………………………….

Additional information: e.g. physical defects, infection, chronic or family diseases etc.
……………………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………………

I certify that the above is fit to pursue further studies. Signature ………………………………………………..

Designation ………………………………………………..

Station ……………………………………………..…

Date: ……………………………………..…………

**SHULE YA SEKONDARI NAMWAI**

**FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

1. JINA ………………………………………………………………………………………… DINI …………………………………………........

2. TAREHE YA KUZALIWA………………………………………………..3. KIJIJI ULIMOZALIWA……………………………..

4. TARAFA ULIMOZALIWA ……………………………………………..5. WILAYA ULIMOZALIWA ………………………….

6. MKOA ULIMOZALIWA ……………………………………………….. KAMA UNAKAA MJINI TAJA ……………………….

8. JINA LA BABA…………………………………………………………….9. KAZI YA BABA……………………………………….

10. ANWANI YA BABA……………………………………………………………NAMBA ZA SIMU ……………………………….

11. JINA LA MAMA ……………………………………………………. 12. KAZI YA MAMA……………………………………..

13. ANWANI YA MAMA……………………………………………………NAMBA ZA SIMU …………………………………….

14. JINA LA ATAKAYEHUSIKA NA MWANAFUNZI KIPINDI CHOTE CHA MASOMO:
JINA:…………………………………………………… ANWANI:……………………………………………………………
SIMU:………………………………………………… EMAIL: ……………………………………… ………………

15. SHULE ULIZOSOMA MADARASA MADARAKA ULIYOSHIKA

| SHULE ULIZOSOMA | MADARASA | MADARAKA ULIYOSHIKA |
|---|---|---|
| ……………………………………… | ……………………………… | …………………………………………… |
| ……………………………………… | ……………………………… | …………………………………………… |

16. JE, BABA YU HAI? ………………………………… (NDIYO/HAPANA)

17. JE, MAMA YU HAI? ………………………………… (NDIYO/HAPANA)

18. JE, UNAKAA NA MLEZI …………………………… (NDIYO/HAPANA) JINA LA MLEZI ……………………………

19. ANWANI YA MLEZI …………………………………………NAMBA ZA SIMU…………………………………………

20. KAZI YA MLEZI …………………………………………………………………………

23. ELEZA MIPANGO YAKO YA MAISHA YA BAADAYE
…………………………………………………………………………………………………………………………………

25. KAZI AMBAZO UNGEPENDA KUFANYA BAADA YA KUMALIZA MASOMO
…………………………………………………………………………………………………………………………………

26 KAZI AMBAZO USINGEPENDA KUFANYA BAADA YA KUMALIZA MASOMO
…………………………………………………………………………………………………………………………………

26. JINA LA MWANAFUNZI ………………………………… SAHIHI………………………TAREHE…………………………